Ombi la Kurekebisha Bei za Maji kwa Miaka Mitatu la

MAMLAKA YA MAJISAFI NA MAJITAKA TANGA (TANGA UWASA)

Utangulizi

1. Mnamo tarehe 4 Septemba 2012, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (“EWURA”) ilipokea maombi kutoka Mamlaka ya Majisafi na Majitaka ya Tanga ("Tanga UWASA") kwa ajili ya marekebisho ya bei za maji kwa miaka mitatu toka 2012/13 hadi 2014/15 kwa ajili ya mapitio na maidhinisho. Tanga UWASA iliomba:

(a) kuongeza bei kutoka wastani wa Shilingi 575 kwa mita ya ujazo ya sasa hadi Shilingi 964 kwa mita moja ya ujazo kwa mwaka 2012/13, Shilingi 1,071 kwa mwaka 2013/14 na Shilingi 1,094 kwa mwaka 2014/15;

(b) kuongeza bei ya majitaka kwa kiwango cha asilimia kati ya 13.6 na 33.3 kwa mwaka 2012/13 na bei hiyo iliyoongezeka kuendelea kutumika katika mwaka 2013/14 na mwaka 2014/15;

(c) kuongeza tozo za huduma kwa kiwango cha kati ya asilimia 16.7 na 25 kwa mwaka 2012/13 na tozo hiyo iliyoongezeka kuendelea kutumika katika mwaka 2013/14 na mwaka 2014/15;

(d) kuongeza tozo za maunganisho mapya ya maji kwa wastani wa asilimia 39 ifikapo Juni 2014/15;

(e) kuendelea kutoza ada ya marejesho ya huduma ya maji ya asilimia 10 ya deni;

(f) kuongeza ada ya maunganisho ya huduma ya majitaka kutoka Shilingi 10,000 hadi 50,000 kwa mwaka 2012/13 na ada hiyo iliyoongezeka kuendelea kutumika katika mwaka 2013/14 na mwaka 2014/15; na

(g) bei iliyopendekezwa ianze kutumika kuanzia tarehe 1 Oktoba 2012.

Sababu ya Kurekebisha Bei

2. Sababu ilizotolewa na Tanga UWASA kuhusu mapendekezo ya bei na tozo ni kuiwezesha Mamlaka hiyo kupata mapato ya kutosha ili kumudu kulipia gharama za uendeshaji na matengenezo katika kutoa huduma na kulipia gharama za uwekezaji. Kuongezeka kwa mapato kutaiwezesha Tanga UWASA kufanya ukarabati wa miundombinu na kuondoa mabomba yaliyochakaa ili kupunguza tatizo la mivujo ya maji. Sababu nyingine iliyotolewa na Tanga UWASA ni kuongezeka kwa gharama za watumishi kutokana na kupitia upya muundo wa utumishi wa mamlaka na mpango wa mamlaka wa kuongeza idadi ya watumishi. Aidha ongezeko hilo litaiwezesha Tanga UWASA kutekeleza mpango wake wa kibiashara wa miaka mitatu ambao umeweka vipaumbele katika miradi mbalimbali ya maendeleo.

Ushirikishwaji wa Wadau

3. Kwa mujibu wa kifungu cha 19(2) (h) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Sura ya 414, EWURA ilifanya taftishi kuhusu uhalali wa ombi la kurekebisha bei zilizopendekezwa. Taftishi hiyo ilihusisha tathmini ya masuala ya kiuchumi na ya kiufundi pamoja na kukusanya maoni kutoka kwa wadau katika mkutano uliofanyika katika Jiji la Tanga mnamo tarehe 30 Oktoba 2012.

4. Wakati wa taftishi, wadau wakiwemo, Baraza la Ushauri la Serikali (*Government Consultative Council* ("GCC")), na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma zinazodhibitiwa na EWURA (*Consumers Consultative Council* ("EWURA CCC")) walikutana ili kuchunguza na kutoa hoja zao kuhusu uhalali wa maombi hayo. Wananchi pia walipata fursa ya kuwasilisha EWURA hoja zao kwa maandishi.

5. GCC walihoji, pamoja na mambo mengine, kuhusu kiwango kikubwa cha upotevu wa maji, gharama kubwa za watumishi na ubora duni wa maji ambao hauendani na viwango vinavyokubalika.

6. EWURA CCC walihoji, pamoja na mambo mengine, kuhusu kutokuwa na mgawanyika mzuri wa gharama za uwekezaji katika kipindi cha miaka mitatu, gharama kubwa za maunganisho ya majisafi na kukosekana viambatanisho vinavyoonyesha mchanganuo wa namna gharama za utumishi zilivyoongezeka.

7. Wananchi walihoji, pamoja na mambo mengine, sababu za kutozwa tozo ya huduma (service charge), bei kubwa iliyopendekezwa, ubora duni wa mabomba ya maunganisho ya majisafi na ukosefu wa huduma ya majisafi eneo la Mapojoni.

8. Wakati wa kuhitimisha taftishi tarehe 13 Novemba 2012, EWURA ilipokea maoni ya kutosha kuweza kufanya maamuzi.

Uchambuzi na marekebisho

9. Kufuatia kukamilika kwa mchakato wa taftishi na uchambuzi, EWURA imefikia uamuzi kwamba ombi la marekebisho ya bei na tozo la Tanga UWASA lina mantiki na ni halali isipokuwa viwango vikubwa vya bei ya majisafi vilivyopendekezwa. Vilevile mapendekezo ya bei ya mwaka 2014/15 yamekataliwa kutokana na Mpango wa Kibiashara wa mamlaka kumalizika mwaka 2013/14.

10. Marekebisho ya Mahitaji ya Mapato kwa Tanga UWASA kwa mwaka 2012/13 hadi mwaka 2013/14 ni kama yanavyooneshwa katika Jedwali hapa chini:

Jedwali 1: Marekebisho ya Mahitaji ya Mapato

	Makisio	**Makisio**
	2012/13	**2013/14**
Gharama za Huduma	**TZS**	**TZS**
Gharama za Uzalishaji	730,872,643	790,589,859
Gharama za Usambazaji	245,383,310	261,461,384
Gharama za Ukarabati na Matengenezo	332,215,825	355,047,144
Gharama za kuondoa Majitaka	39,687,676	42,415,187
Gharama Utumishi	1,881,968,887	2,273,741,079
Gharama za Utawala	1,222,379,086	1,232,527,549
Gharama za Bodi	104,889,551	112,098,019
Gharama za EWURA	60,836,397	73,858,755
Ada mbali mbali	92,270,448	98,611,675
Gharama za mkopo	15,378,353	29,193,938
Gharama za kujitangaza kibiashara	60,206,391	64,344,037
Gharama za matukio mbalimbali	41,620,012	44,480,321
Gharama za Kifedha	14,955,461	15,983,266
Gharama nyinginezo	105,757,153	113,025,245
Jumla ya Gharama za Uendeshaji na Matengenezo	**5,232,767,202**	**5,492,739,277**
Gharama za Uchakavu wa Mitambo	1,261,358,983	1,234,595,076
Gharama za uwekezaji	1,279,720,503	1,388,960,667
Jumla ya Mahitaji	**7,773,846,688**	**8,116,295,020**

Uamuzi

11. Katika kikao chake cha tarehe 19 Desemba 2012, Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA ilijadili ombi hili na kutoa maamuzi kama inavyoonyeshwa kwenye Agizo hapa chini:

SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA

(SURA NA 272)

AGIZO Na. -----

(Imetolewa kwa mujibu wa Kifungu Na.28 (d) cha Sheria ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, 2009)

MAMLAKA YA MAJISAFI NA MAJITAKA TANGA ("TANGA UWASA"), AGIZO LA KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJI, 2012

Kichwa cha Agizo

1. Agizo hili litajulikana kama, Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Tanga ("Tanga UWASA"), Agizo la Kurekebisha Bei za Huduma ya Maji, 2012.

Tarehe ya Kuanza

2. Agizo hili litaanza kutekelezwa rasmi kuanzia tarehe 1 Januari, 2013.

Marekebisho ya Bei

3. Bei za majisafi na majitaka za Tanga UWASA zinarekebishwa kulingana na Jedwali la Kwanza lililopo katika Agizo hili.

Masharti

4. Bei zilizopitishwa zitaambatana na masharti yafuatayo:

(a) ifikapo tarehe 30 Juni, 2013 au kabla, Tanga UWASA inatakiwa iwe imewasilisha EWURA taarifa ya kina ya mpango wa kuimarisha mahusiano, mawasiliano, utoaji habari na uelimishaji wa wateja (customer outreach programme) kwa mwaka 2013/14;

(b) Tanga UWASA itatekeleza miradi iliyooneshwa kwenye Jedwali la Pili la Agizo hili kwa kutumia fedha zitakazotokana na bei zilizoidhinishwa;

(c) EWURA inaweza kurekebisha bei za Tanga UWASA za mwaka 2013/14 ambapo itathibitika kuwa hapakuwepo na sababu za Tanga UWASA kushindwa kutekeleza miradi ya mwaka wa 2012/13 kulingana na ratiba iliyo kwenye Jedwali la Pili la Agizo hili. Marekebisho ya bei yatakuwa sawa na makadirio ya gharama ya miradi ambayo haikutekelezwa;

(d) Tanga UWASA itafikia viashiria vya utendaji kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Tatu la Agizo hili;

(e) EWURA inaweza kuanzisha usimamizi maalum kwa Tanga UWASA kama haitafikia mojawapo ya viashiria vya utendaji kwa mwaka wa 2012/13 na 2013/14 kama ilivyobainishwa kwenye Jedwali la Tatu la Agizo hili. Usimamizi maalum unajumuisha kuitaka Tanga UWASA kuongeza ripoti za utendaji inazowasilisha EWURA na EWURA kuongeza ufuatiliaji wa utendaji wa Tanga UWASA;

(f) Tanga UWASA itaendelea kuwasilisha kwa EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa mwongozo wa EWURA. Taarifa hizi zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Tanga UWASA ikilinganishwa na vyombo vingine vya utoaji wa huduma za maji na uboreshaji wa huduma zake. EWURA itazingatia tathmini hii katika kufanya maamuzi ya maombi yote yatakayowasilishwa na Tanga UWASA katika siku zijazo; na

(g) ifikapo tarehe 31 Machi 2013 au kabla, Tanga UWASA inatakiwa iwe imewasilisha EWURA Mpango wake wa Kibiashara uliopitiwa upya na kujumuisha masharti ya Agizo hili.

5. Agizo hili limetengua Agizo Na. 12-011 la tarehe 15 Machi 2012 la Kurekebisha Bei za Majisafi na Majitaka kwa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Tanga (Tanga UWASA).

MAJEDWALI

JEDWALI LA KWANZA: BEI ZILIZOIDHINISHWA

Jedwali 1(a): Bei ya Maji

Kundi la Wateja	Kundi la Matumizi (m^3)	Bei ya Sasa (TZS/m^3)	Bei Iliyoombwa (TZS/m^3)		Bei Iliyoidhinishwa (TZS/m^3)	
			2012/13	2013/14	2012/13	2013/14
Majumbani	0 - 5	565	820	910	700	680
	>5 -10	565	870	970	750	720
	>10-30	565	950	1,060	800	790
	>30	565	1,100	1,200	950	910
Taasisi	0 - 5	565	820	910	700	680
	>5 -10	565	870	970	750	720
	>10-30	565	950	1,060	820	790
	>30	565	1,100	1,200	950	910
Biashara	0-10	620	1,000	1,110	860	830
	>10-30	620	1,100	1,210	950	910
	>30	620	1,200	1,290	1030	990
Viwanda	0-30	740	1,100	1,200	950	900
	>30	740	1,300	1,330	1100	1070
Magati		6.2	700	775	TZS 10/lita 20	TZS 10/lita 20
Wateja wa jumla		670	1,000	1,240	860	830

Jedwali 1(b): Bei ya Majitaka

Kundi la Wateja	Bei ya Sasa (TZS/m^3)	Bei Iliyoombwa (TZS/m^3)		Bei Iliyoidhinishwa (TZS/m^3)	
		2012/13	2013/14	2012/13	2013/14
Majumbani	120	150	150	150	150
Taasisi	220	250	250	250	250
Biashara	225	300	300	278	278
Viwanda	302	350	350	302	302

Jedwali 1(c): Tozo ya Huduma (Service Charge)

Kundi la Wateja	Tozo ya Sasa (TZS/ Mwezi)	Tozo Iliyoombwa (TZS/ Mwezi)		Tozo Iliyoidhinishwa (TZS/ Mwezi)	
		2012/13	2013/14	2012/13	2013/14
Majumbani	1,200	1500	1500	1500	1500
Taasisi	2,000	2500	2500	2400	2400
Biashara	2,000	2500	2500	2400	2400
Viwanda	2,500	3000	3000	3000	3000

Jedwali 1(d): Tozo ya Maunganisho Mapya ya Huduma ya Majisafi

Kundi la wateja	Tozo ya sasa (TZS)	Tozo Iliyoombwa (TZS)		Tozo Iliyoidhinishwa (TZS)	
		2012/13	2013/14	2012/13	2013/14
Majumbani	180,000	180,000	180,000	Tozo ya Maunganisho mapya ni kama ilivyoainishwa kwenye Kanuni za Sheria ya Maji za Mwaka 1997 Kifungu Na 12(3)	
Taasisi	180,000	180,000	180,000		
Biashara	180,000	180,000	180,000		
Viwanda	180,000	180,000	180,000		

Jedwali 1(e): Ada ya Kurejesha Huduma ya Maji Baada ya Kusitishwa

Kundi la Wateja	Ada ya sasa (TZS)	Ada Iliyoombwa (TZS)		Ada Iliyoidhinishwa (TZS)	
		2012/13	2013/14	2012/13	2013/14
Majumbani	Asilimia 10 ya deni	Asilimia 10 ya deni	Asilimia 10 ya deni	10,000	10,500
Taasisi	Asilimia 10 ya deni	Asilimia 10 ya deni	Asilimia 10 ya deni	14,000	15,000
Biashara	Asilimia 10 ya deni	Asilimia 10 ya deni	Asilimia 10 ya deni	15,000	15,500
Viwanda	Asilimia 10 ya deni	Asilimia 10 ya deni	Asilimia 10 ya deni	20,000	21,500

Jedwali 1(f): Ada ya Maunganisho ya Huduma ya Majitaka

Kundi la Wateja	Ada ya sasa (TZS)	Ada Iliyoombwa (TZS)		Ada Iliyoidhinishwa (TZS)	
		2012/13	2013/14	2012/13	2013/14
Majumbani	10,000	50,000	50,000	Ada ya Maunganisho mapya ni kama ilivyoainishwa kwenye Kanuni za Sheria ya Maji za Mwaka 1997 Kifungu Na 12(3)	
Taasisi	10,000	50,000	50,000		
Biashara	10,000	50,000	50,000		
Viwanda	10,000	50,000	50,000		

JEDWALI LA PILI:

MIRADI ITAKAYOTEKELEZWA 2012/13 – 2013/2014

S/N	Maelezo ya Mradi	Kipindi cha Utekelezaji	
		Juni 2013	Juni 2014
A.	**MIRADI YA KUDHIBITI MIVUJO YA MAJI**		
1.	Ukarabati wa mabomba chakavu	Kilomita 11.3 kwenye maeneo mbalimbali	Kilomita 24.9 kwenye maeneo mbalimbali
2.	Ununuzi na ufungaji wa valvu za kurekebisha msukumo wa maji	Valvu 2	Valvu 3
3.	Kulaza mabomba ili kupunguza urefu wa mabomba ya kuwaunganisha wateja	Km 5	Km15
4.	Ununuzi wa dira kuu za maji	Dira 4	Dira 5
B.	**MIRADI YA UKARABATI**		
1.	Kubadilisha mabomba yaliyochakaa ya majitaka	Km 0.3 eneo la Ngamiani	Km 0.337 eneo la Ngamiani
2.	Upakaji Majengo Rangi	Maji ya mitambo ya kusafisha maji Mowe, Nyumba za watumishi Mowe na jengo la kituo cha kusukuma maji Maweni	
3.	Kubadilisha dira za wateja	Dira 1200	Dira 1250
4.	Ukarabati wa Uzio	Kituo cha kusukuma maji Kange	
5.	Ukarabati wa jingo la ofisi	Jengo la ofisi za Gofu namba 1 na 2	Kubadilisha paa la eneo la kupaki magari-Mabayani
6.	Kuondoa mabomba sehemu zisizoruhusiwa (No trespass properties)	Km 11.37 maeneo ya Kwakaeza, Sahare, Chumbageni na Maeneo mengine	Km 23.61 maeneo ya Kwakaeza, Sahare, Chumbageni na Maeneo mengine
C.	**Miradi ya Uwekezaji**		
1.	Upanuzi wa mtandao wa majisafi	Km 17.9 kwenye maeneo ya Kange, Mkulumuzi,Masiwani, Mwakidila	Km 23.8 kwenye maeneo ya Kange, Mkulumuzi,Masiwani, Mwakidila
2.	Kujenga chemba za majitaka	Chemba 5	Chemba 9
3.	Upanuzi wa mtandao wa majitaka	Km 0.430 kwenye mitaa namba 5, 21 na 13.	Km 0.750km kutoka kituo cha treni hadi Chuda
4.	Uboreshaji wa msukumo na	Km 1.3 kwenye maeneo	Km 1.3 kwenye maeneo

S/N	Maelezo ya Mradi	Kipindi cha Utekelezaji	
		Juni 2013	Juni 2014
	mzunguko wa maji kwenye mtandao	ya Mwahako, Kwaminchi, Mabawa, Chumbageni na mengine	ya Mwahako, Kwaminchi, Mabawa, Chumbageni na mengine
5.	Ujenzi wa choo cha maji	Kituo cha kusukuma maji Maweni	
6.	Kununua viwanja kwa ajili ya kujenga ofisi na eneo la kujenga eneo la mabwawa ya majitaka	Moja eneo la Duga. Moja eneo la Pongwe	Ununuzi wa ardhi eneo la Machui kwa ajili ya kujenga mabwawa ya majitaka
7.	Ujenzi ya nyumba ya madawa ya kusafisha maji na Maabara	Ujenzi wa nyumba moja eneo la mitambo ya Mowe	Ujenzi na ufungaji vifaa vya maabara kwenye mitambo ya maji Mowe

JEDWALI LA TATU

VIASHIRIA VYA UTENDAJI (2012/13 – 2013/14)

Na	Maelezo	Kipimo	Viashiria	
			2012/13	2013/14
1.	Idadi ya wateja wapya maji safi	Namba	1795	1647
2.	Idadi ya wateja wapya maji taka	Namba	50	50
3.	Ubora wa Maji			
	Turbidity	%	100	100
	E-Coli	%	98.5	100
4.	Kiwango cha upotevu wa Maji	%	24.5	24
5.	Kiwango cha kujibu malalamiko ya wateja yaliwasilishwa kwa maandishi	%	100	100
6.	Gharama za utumishi kama sehemu ya maduhuli ya majisafi na majitaka.	%	30	30

Dar es Salaam HARUNA MASEBU

Mkurugenzi Mkuu

19 Desemba 2012